# *Umoja Wa Muungano*

. . .furaha kuwa na majaliwa ya kuja katika Uwepo Wako na kukutana na Wewe. Na, Ee Mungu, na tuwe na ushirika usiku wa leo kwenye Neno lililoandikwa. Jalia Roho Mtakatifu avuvie yote yanayofanywa au kusemwa. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

2 Karibu wanishike bila kujua. Nilikuwa nikimwangalia chini hapa maskini ndugu wa Arkansas kutoka huko chini kabisa katika jimbo hilo kuu la Arkansas. Nawe unafanya nini hapa katika nchi hii baridi hata hivyo?

3 Vema, popote niendapo, ninakutana na watu kutoka Arkansas. Palikuwa mojawapo ya sehemu zangu za kwanza kwenda baada ya kuondoka St. Louis, ambapo tulikuwa kwenye Ukumbi wa Keil, kisha tukashuka kwenda Arkansas. Na kamwe siwasahau watu hao, jinsi walivyokuja. Loo, ninii tu, kulikuwako na watu ishirini na nane elfu; gazeti lilisema, huko Jonesboro. Nao mji huo una yapata elfu nane ama kumi, nadhani, idadi ya watu. Kwa maili thelathini kuuzunguka huo mji, hakukuwako na kitu; nyumba zote za mashambani zilichukuliwa, na mahema kupigwa na kadhalika, na watu wakiishi humo, chini ya ma—malori ya kale. Nao watu, inanyesha . . . Kungekuwa kukinyesha, huku watu wameshikilia vipande vidogo vya turubai na magazeti juu ya jamaa zao wagonjwa, wakingojea tu wapate kuombewa. Haikuleta tofauti yoyote kama waliingia juma hili au juma lijalo. Wakati wowote ule, ingekuwa ni sawa. Mnaona?

4 Nami ninakumbuka huko chini Corning. Unaishi karibu na huko, sivyo? Corning. Unaonekana . . .Niliona kitu fulani kule ambacho nadhani labda Dwight Moody, ama Sankey, ama baadhi ya hao walikiona katika siku zao.

5 Nilikuwa huko mbali sana nyikani, nilikuwa nimeenda huko nyuma na nilikuwa kule nyuma nikiomba, peke yangu, kabla ya ibada. Ningeona watu wakitoka kwenye barabara hizo za mavumbi, wakishuka kwenda kwenye ibada, wakati wa alasiri. Nami nikawaona wasichana wadogo, wasichana warembo, wasiozidi umri wa miaka kumi na sita, kumi na minane, wamebeba viatu vyao na soksi ndefu chini ya mikono yao. Kabla hawajafika huko, wangeketi chini, wapanguse mavumbi miguuni mwao, na kuvaa soksi zao na viatu vyao. Walikuwa na jozi moja tu, na ilibidi idumu. Lakini walimpenda Bwana kweli.

6 Baadhi ya miujiza mikubwa sana ambayo nimewahi kuona ikifanywa Marekani ilifanyika huko. Nami ninataka kurudi Arkansas, moja ya siku hizi, kuwa tu na ushirika wa mtindo wa kale kwenye Neno na watu wa Mungu.

7 Sasa, tuko mapema kidogo, usiku wa leo, na kwa hiyo tutasoma baadhi ya Neno la Milele la Mungu, kama kawaida. Nami nataka kuninii . . .

8 Aisee, naamini walisema, hapa, tulikuwa na . . . (Mmekwisha kutangaza hicho kifungua kinywa cha wahudumu, na kadhalika?) [Ndugu mmoja anasema, "Naam."—Mh.] Naam. Sawa. Hilo ni sawa, basi.

9 Tunataka kusoma usiku wa leo kutoka katika Kitabu cha Mwanzo. Nami ninawatakeni msikilize tunaposoma kutoka kwenye mlango wa 11 na kifungu cha 5.

> *BWANA akashuka ili auone mji na mnara, waliokuwa* wameujenga *wana wa wanadamu.*
>
> *BWANA akasema, Tazama, watu hawa* ni *ninii moja,* . . .

10 Ninataka kuzungumza, usiku wa leo, juu ya *Umoja wa Muungano*, sasa, tunapoingia moja kwa moja kwenye Neno, kwa ajili ya maonyo haya. Na sasa mimi . . . Inashangaza sana, kuwazia kwamba, jinsi ambavyo watu walivyoona hapa walikuwa mmoja.

11 Na, mnajua, huo ndio mpango wa Mungu, Mungu anataka watu wawe kitu kimoja. Na ni ajabu kuwazia, lakini ibilisi hujaribu kufanikisha mpango wake na kuwafanya watu kuwa kitu kimoja chini ya mpango wake. Sasa, Mungu ana mpango, naye ibilisi ana mpango. Halafu basi ibilisi anajaribu kuwaweka watu wote chini ya mpango wake, wakati Mungu anajaribu kuwafanya watu wawe kitu kimoja chini ya mpango Wake.

12 Kwa hiyo kuna roho mbili kuu ulimwenguni, moja yazo ni ibilisi, nyingine ni Mungu. Ibilisi ana wajumbe, Mungu ana wajumbe, nasi tuko huru kufanya chaguo letu. Yule ambaye tutajisalimisha kwake, huyo ndiye tulio watumishi wake. Lakini kama ukiangalia wakati . . .

13 Nilikuwa nikihubiri Jumapili iliyopita juu ya kiu iliyo ndani ya watu, mwanadamu. Mungu alimfanya mwanadamu kuona kiu, ila ni kumwonea Yeye kiu. Ndiyo maana kiu iliwekwa katika mwanadamu.

14 Lakini ibilisi hunyemelea na kukipotosha hicho, na kuwafanya watu wamwonee kiu, kwa mambo ya ulimwengu. Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yako." Ndipo, mnaona, ibilisi hupotosha. Hawezi kuumba chochote, lakini anaweza kupotosha kile Mungu ameumba tayari. Ibilisi si muumbaji. Yeye ni mpotoshaji tu wa uumbaji wa asili. Nayo dhambi ni nini? Ni haki iliyopotoshwa.

Ni wangapi wanaelewa hilo? Mnaona? Vema. Nashangaa tu.

15 Mimi ni mtu wa Kusini, nasi tumezoea tu majibu zaidi ya hayo. Na—nao watu wa Kaskazini hawapendi mabadiliko. Na—

nami nimekuwa Kusini kwa muda mrefu sana hata inabidi tu mzoee njia zangu za Kusini, ama mimi njia zenu za Kiyankii.

16 Lakini nawatakeni mjue, tulishinda vile vita. Naam. Hatuna ubishi juu ya hilo. Kuna mtu mmoja wa Kusini aliye hai, wala hakuna Mayankii, kwa hiyo tulishinda vita. Niliwazia ilikuwa ya kushangaza zaidi wakati maskini yule Yankii alipokuwa akifa, hata hivyo, naye yule Mkusini akamtumia telegramu na kusema, "Mungu akubariki, Yankii. Natumaini kukuona tena, hivi karibuni." Hiyo, kwa nini hawakufikiria jambo hilo hapo mwanzo, mnaona, na kuliachilia tu? Lakini napenda kusema hivyo, kwamba kuna ninii tu. . . Ilichukua muda wa maisha, kushinda hivyo vita, lakini hatimaye tukaupata. Mnaona? Vema. Lakini kuna wakati mzuri sana unaokuja.

17 Na sasa tukizungumza juu ya—ya adui, jinsi anavyopotosha uadilifu kuwa udhalimu. Sasa, hilo, sisi ni kundi lililochanganyikana, wanaume na wanawake pia, wengi ni watu wazima, kwa hiyo nina hakika mtaelewa. Nyinyi humsikiliza daktari wenu, nami ni ndugu yenu. Ni halali, na ya haki, na ya kitauwa, kwa mwanamume kujitwalia mke, na kuishi na mke huyu. Lakini mwanamke mwingine anaweza kuwa kitu kile kile kwake, lakini ingekuwa ni kifo kumgusa. Hiyo hapo tofauti yake, haki iliyopotoshwa. Hivyo ndivyo dhambi yote ilivyo, ni haki iliyopotoshwa.

18 Mungu alikufanya umwonee Yeye kiu, pia Mungu alilifanya Kanisa liwe na umoja chini ya utawala Wake. Lakini ibilisi huwafanya wawe na umoja chini ya milki yake.

19 Na sasa kama utaangalia katika dini ya Kiislamu, baadhi ya mambo hayo, laiti tungeweza kuchukua wakati. Mambo yaliyopo, jinsi yamepotoshwa! Katika dini ya Kiislamu, ambayo nimekuwa na majaliwa ya kuzuru nchi iliyo karibu na kaburi la Muhammad, basi kwenye kaburi lake kumekuwa farasi mweupe amesimama pale kwa miaka elfu mbili. Kila saa nne, nafikiri ndivyo, wanabadilisha mlinzi, na farasi mweupe, aliyetandikwa, huku akingojea kufufuka kwa Muhammad. Nao wanasema ya kwamba atafufuka katika wafu, ampande huyu farasi, na kuushinda ulimwengu.

20 Basi, mnaona, wanamngojea mshindi aje, amepanda farasi mweupe, na jinsi hilo limepotoshwa kutoka kwa Maandiko. Kwa sababu, "Yesu yuaja, amepanda farasi mweupe, vazi Lake lililochovywa katika damu; Jina Lake, Neno la Mungu." Lakini, mnaona, ibilisi alichukua nadharia hiyo na kuipotosha kwa Muhammad. Lakini, kwa kweli, Yesu atakuja juu ya farasi mweupe. Biblia inasema kwamba atakuja.

21 Basi unaweza kuingia katika dhehebu lolote la uongo utakalo na utaona alama nyingi kuu za Ukristo wa kweli.

22 Sasa, katika ule mnara wa Babeli, kama ukiangalia huo mnara, ulikuwa ni mwanzo wa Babeli; ambayo nitaizungumzia

baadaye juma hili, Bwana akipenda. Babeli, huo mji wenyewe, ulifanywa kwa mfano wa Mbinguni. Na humo ndani walikuwa na mto Frati ukitiririka moja kwa moja karibu na kiti cha enzi na bustani, bustani inayopembea. Na hiyo ilifanywa kwa mfano wa Mbingu, kwa kuwa Mto wa Uzima, Ki-. . .unapitia karibu na Kiti cha Enzi cha Mungu. Nanyi mnaona mafanikio ambayo mwanadamu alikuwa akipata, yalikuwa ni ya kufananisha, upotovu.

23 Halafu basi, katika jambo hili kuu, walikuwa na mtu jina lake Nimrodi. Kisha Nimrodi akaifanya miji yote iliyosalia na taifa kuwa chini ya mamlaka moja kuu, ikionyesha kwamba ni nadharia iliyobuniwa na mwanadamu, mfano tu.

24 Lakini Kanisa la Mungu limeunganishwa chini ya Mungu. Mwanadamu hana uhusiano wowote Nalo. Limeunganishwa chini ya Mungu.

25 Na Babeli hii, ambayo ilikuwa mwanzo wa. . .Katika uumbaji, katika Mwanzo, tunaona ya kwamba iko moja kwa moja katika Ufunuo, na inazungumza juu ya ulimwengu wake wa kikanisa katika siku za mwisho, ambazo ni sasa, hatimaye itaungana chini ya mpinga-Kristo, dini ya kujibunia.

26 Lakini ninashukuru kusema kwamba Kanisa la Mungu litaunganishwa, pia, chini ya Kichwa kimoja, Mungu.

27 Lakini dini za kujibunia zote zitaingia katika dini hii ya mpinga-kristo. Kutakuwa na aina zake mbili. Aina moja itatoka Rumi, ambayo itakuwa ni yule mnyama. Na kuna sanamu ya mnyama, ambayo itakuwa ni kiongozi wa kikanisa wa kanisa la Kiprotestanti, ikusanyike kama sanamu ya mnyama, chini ya ulimwengu wa kimadhehebu. Nayo yote yatakuja chini ya utawala mmoja mkuu, na mpinga-Kristo ndiye atakayetawazwa na kuketishwa. *Mpinga*, "dhidi ya," karibu kufanana kabisa, lakini hata hivyo mafundisho ya—ya—yake hayatokani na Maandiko. Maandiko ya kutosha kuyafanya yaonekane kama ni ya kweli, lakini yatakuwa ni ya uongo.

28 Nami najua mna—mnasema, "Ndugu Branham, unarejea Rumi sasa." Hiyo ni kweli hasa. Wala si Rumi tu, bali Uprotestanti, pia. Hasa. Biblia ilisema hivyo.

29 Lakini haya basi, ibilisi akiwaunganisha watu chini ya kichwa kimoja, kichwa kimoja cha kikanisa, mtu mmoja duniani. Biblia ilisema, "Angeketi katika hekalu la Mungu, akionyesha kwamba yeye ni Mungu." Na jinsi angevaa taji yenye sehemu tatu, na mambo haya yote ambayo angefanya, "Halifa wa—wa mbingu, dunia, na toharani." Na chini ya huu kutakuwa na sa—sanamu kwake, ambapo wengine wote wangeungana pamoja.

30 Lakini Kanisa la Mungu aliye hai litaunganishwa chini ya nguvu za Mungu na uangalizi wa Roho Mtakatifu. Kanisa la Mungu litaungana. Loo, hivi hamna furaha?

31 Katika saa hii ya giza, wakati kila kitu kinazimika, watu hawajali. Hawajali. Ilionekana kana kwamba mioyo yao inaenda mbali zaidi na zaidi na Mungu. Ulimwengu unaendelea kuwa baridi zaidi na zaidi, na kutojali, kwa sababu hawa viongozi wa kikanisa wanaungana.

32 Huko Urusi, Urusi inajaribu kuunganisha ulimwengu chini ya ukomunisti, Urusi. Ibilisi anayeitawala Urusi anajaribu kuunganisha ulimwengu wote chini ya ukomunisti. Kamwe hawatafaulu.

33 Halafu U.N., Umoja wa Mataifa, unajaribu kuwaunganisha chini ya muungano wa kikosi cha polisi, mfumo mwingine wa kujibunia. Hautafanikiwa kamwe. Hauwezi. Lakini wote wanajaribu.

34 Na hebu niseme hivi kwa heshima, bali kulingana na Neno la Mungu, kwamba kila taifa siku hizi linatawaliwa na ibilisi. Biblia ilisema hivyo. Shetani alimwonyesha Bwana wetu falme za ulimwengu, naye akasema, “Hizi zote ni zangu, kufanya nazo chochote nipendacho. Basi kama utanisujudia, nitakupa Wewe zote.”

35 Naye Yesu alijua ya kwamba atazirithi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa hiyo akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani.”

36 Kama ulimwengu ulitawaliwa na Kristo, tungekusanya silaha wala kusingekuwa na risasi nyingine kufyatuliwa. Hatungekuwa na haja ya masputiniki na mabomu ya haidrojeni, kuwalipua watu. Kristo atakapochukua utawala wa ulimwengu huu, kama “Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana,” watu wataunganishwa Naye, chini ya milki moja kubwa. Itakuwa wakati wa ajabu!

37 Mataifa yote yanataka watu wawe kitu kimoja. Ujerumani ilidhani wote walipaswa kuwa Wajerumani. Urusi inafikiri wote wanapaswa kuwa Warusi. Ulimwengu wa Magharibi unafikiri wote wanapaswa kuja huku. Nao wanawataka waongee lugha moja, kama tu walivyofanya huko Babeli. Mungu alisema, “Wao ni lugha moja.” Naye anataka wote wazungumze lugha moja. Wanataka wote wawe watu wamoja walioungana, lakini kamwe halitatendeka chini ya himaya ya mwanadamu.

38 Lakini nitasema hivi, ya kuwa wakati unakuja ambapo mataifa yote yataungana pamoja chini ya Mfalme mmoja, na huyo atakuwa ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Nao watazungumza lugha moja. Watakuwa wenye moyo mmoja na nia moja. Danieli aliuona mwisho, wakati lile Jiwe lilipochongwa kutoka mlimani, bila kazi ya mikono, Nalo likafingirikia kwenye falme za ulimwengu, na kuzivunjilia mbali, nazo zikawa kama takataka sakafuni, makapi ambayo upepo uliyapeperushia mbali. Lakini hilo Jiwe liliifunika dunia nzima. Jiwe hilo ni Kristo. Kutakuwa na wakati kutakuwako na

taifa moja, watu wamoja, bendera moja: ule msalaba wa kale unaoparuza. Mungu aliye hai na asifiwe!

> Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote
> Ila Damu ya Yesu na haki;
> Wakati yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka,
> Basi Yeye ndiye tumaini langu na nanga yangu.
>
> Kwa kuwa kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

39 Sakafu zingine zote, makanisa, madhehebu, mataifa, ma-U.N., chochote kile, yote ni mchanga udidimiao, hayana budi kufikia mwisho wake.

40 Nimekuwa na fursa ya kusimama huko Rumi, ambapo yule Kaisari mkuu aliyejaribu kuunganisha ulimwengu wote chini ya himaya ya Kirumi. Na, leo hii, inakubidi kuchimba futi ishirini kwenda chini, kupata magofu ya mji huo.

41 Nilisimama huko Misri, ambako wale mafarao wakuu walijaribu kuunganisha ulimwengu chini ya Misri, na unachimba futi ishirini na thelathini, kupata magofu ya huo mji. “Kwa maana hapa hatuna mji udumuo,” inasema Biblia, “bali twautafuta Ule ujao.”

42 Si muda mrefu uliopita, wakati wakati mmoja nilipotoka kwenda mahali fulani nilipokuwa mvulana mdogo. Niliona mti mkubwa mno, ambapo nilikuwa nikienda na kuketi chini ya mti huo. Nami nikasema, “Nitakapokuwa mzee, nitarudi na kuketi chini ya mti fulani huu, nami nitaangalia juu kwenye matawi yake. Nitaufurahia uzuri wake, kama nilivyo leo, mvulana wa miaka kumi na miwili.” Hakuna kitu kilichosalia cha mti huo ila kisiki. Kwa nini? Hakuna kitu hapa kinachoweza kuendelea. Hakina budi kikome.

43 Na kila kitu kinachopatikana na mauti huzungumza juu ya Kimoja kijacho kisichopatikana na mauti, kwa maana kila kitu tunachokiona ni kitendo potovu cha kitu ambacho ni halisi.

44 Ninawafungisha ndoa mume na mke, na kumwona msichana mchanga katika wekundu wa ujana wake, kijana mwanamume huku mabega yake yamerudishwa nyuma, wamesimama jinsi walivyo, wamoja, na mioyo yao ikipiga pamoja. Nawazia, “Je, hiyo si ni picha nzuri sana kuweza kuharibiwa na kifo kamwe?” Lakini ni miaka michache tu hadi nywele zao zinaingia mvi, mabega yanainama, na hao wanarudi mavumbini. Ni kitu gani? Ni picha, wanaposimama pale, ya kwamba kuna Nchi ng’ambo ya Mto, ambapo kila dalili ya kifo inaondolewa. Huko, wasiopatikana na mauti, watasimama katika mfano Wake, wakang’ae kuliko jua na nyota.

45 Nyota hiyo kuu ya asubuhi haijapoteza uzuri wake wowote tangu Bwana alipoipuliza kutoka mikononi Mwake na kuitundika katika mzingo wake, halafu angalia kile miaka michache inatufanyia sisi. Lakini Yeye alisema nini katika Maandiko? Alisema, "Hao waliowaongoza wengi kutenda haki watang'aa kuliko nyota." "Kwa hiyo tunautazamia Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni ni Mungu."

46 Baada ya kuona jambo hili kuu ambalo ninajaribu kujenga nia zenu ndani yake, kwa ajili ya somo, ninajaribu kuwafanya mwone huku nje kwamba kuna ku—kutenda kazi kwa adui. Na kutenda kazi kwa adui, kwa roho iliyopotoka, ni kujaribu kufanya yale ambayo Roho wa Kristo anajaribu kufanya. Adui anajaribu, kama ubaya na uzuri, kuunganisha ulimwengu wote chini ya kiongozi mmoja mkuu. Ulimwengu unafanya hivyo; Urusi, U.N. Na sasa acha niende mbele kidogo. Nalo kanisa linajaribu kufanya jambo hilo, chini ya mfumo wa kujibunia. Kamwe hautafaulu. Sio mpango wa Mungu. Ninaweza kuthibitisha hilo kwa Neno Lake.

47 Lakini, mnajua, Mungu alikufanya mtu, kukufanya utamani kuwa hivyo, ili akujaze kwa wema Wake. Sasa, kama. . . Mwanadamu hana budi kujazwa na kitu fulani. Hiyo ni kweli.

48 Huu ni wakati wa kuchagua. Huwezi kuendelea kuwa bila msimamo. Unaweza kuondoka kabla ujumbe huu haujaisha, lakini huwezi kutoka nje ya mlango huo mtu yule yule uliyeingia. Hiyo ni kweli. Utavuka kizingiti hicho, usiku wa leo, ama mtu bora au m—mtu mwovu kuliko ulivyokuwa wakati ulipoingia. Huwezi kuzuia hilo. Ni juu yako kufanya uamuzi. Sasa, angalia, ni wakati wa kuchagua. Huwezi kuwa katikati. Ni wakati wa kuchagua. "Huna budi kuchagua siku hii yule utakayemtumikia." Naye ibilisi amewasilisha mambo mengi, ya mapambo, ambayo unaweza kuyachagua ukipenda. Huwezi kubaki jinsi ulivyo. Kwa sababu, huna budi. . .ikiwa uko tupu.

49 Sasa, ningetaka hili likae miongoni mwetu. Naye Bwana mwema wa Mbinguni anajua ya kwamba sisemi hili nipate kuwa tofauti. Lakini ninasema hivi tu ili kuonyesha Ukweli. Na wainjilisti wetu wakuu ambao wanauvuka ulimwengu siku hizi. . .

50 Na si muda mrefu uliopita, nilipata fursa ya kuketi kwenye kiamsha kinywa pamoja na Billy Graham huyu maarufu, ambaye ninaamini ni mtumishi wa Mungu, akipita katika mataifa, akiwaita kwa Kristo, akiuita ulimwengu kwa Kristo na toba. Ndipo nikamsikia akisema, mbele ya kundi la wahubiri, huku ameiinua Biblia, namna *hii,* naye akasema, "Hii ndiyo—ndiyo mfano." Akasema, "Paulo aliingia kwenye mji na kupata mwongofu. Akarudi mwaka mmoja baadaye na alikuwa na waongofu thelathini." Akasema, "Ninaingia kwenye mji na kupata waongofu elfu ishirini. Ninarudi katika mwaka mmoja

wala sina ishirini." Loo, jinsi nilitaka kusema jambo fulani! Lakini huo ulikuwa ni mkutano wake.

51 Billy Graham, pamoja na ujumbe wake, anawaambia watu watubu na kuachana na dhambi. Na huo ni ujumbe muhimu. Naye Mungu amemchagua Billy Graham kufanya hivyo. Hakuna mtu mwingine anayeweza kufanya kama alivyofanya, kwa sababu anamfuata Bwana. Yeye yuko katika roho ya Yohana, ambayo, kabla ya kuja kwake Kristo mara ya kwanza, alitoka akahubiri toba wala hakufanya miujiza, lakini alihubiri na kuyachochea hayo maeneo na kuwatayarisha kwa ajili ya ujumbe ujao.

52 Lakini, siku hizi, wakati Billy Graham, ndugu yetu mpendwa, anapowafanya watu waachane na dhambi, hana ujumbe wa kuwajaza tena. Hiyo ndiyo shida: umefanywa mtupu.

53 Lakini acha niseme nawe kwa unyenyekevu, kama ndugu yako. Biblia ilisema, "Pepo mchafu akimtoka mtu, hutembea mahali pasipo na maji." Kwa maneno mengine, anazunguka, kila mahali, akijaribu kupata pumziko. Pepo si mbaya sana mpaka ampate mtu ambaye anaweza kuzungumza kupitia au kuishi kwake.

54 Hivi majuzi tu, ningeweza kuhisi pepo huyo mkutanoni. Nanyi nyote mnaotuma barua zenu huku, za kuomba msamaha wa usiku wa kwanza au wa pili, kuamini kwamba ilikuwa ni namna fulani ya njama ya kiakili, na sasa mumeshawishika. Hakika, ninawasamehe. Mungu, amewasamehe, pia. Na Bwana awabariki. Bila shaka.

55 Sasa, wakati mkutano ukiendelea, pepo mchafu mkutanoni, pepo huyo karibu hana madhara mpaka aweze kumshika mtu ambaye anaweza kumtumia. Ndipo anapoweza kumtumia, bila shaka atafanya madhara, kwa sababu yeye ni pepo mchafu.

56 Naye Roho Mtakatifu yuko hapa, akijaribu kutafuta mtu atakayemtumia. Ndipo akipata mtu wa kumtumia, anaweza kufanya mema.

57 Mnaona roho hizo mbili, nia zao, lengo? Angalia jinsi ilivyo. Angalia kazi zao. Angalia matunda yao, ndipo unaweza kuona ni roho gani aliye juu yako. Unahamasishwa na roho. Ikiwa huna roho, umekufa. Na ikiwa una roho, yeye huyahamasisha maisha yako.

58 Na kama maisha yako yanazaa tunda la Kikristo, ni Roho ya Kikristo. Sasa, unaweza kujazwa.

59 Sasa tazama pepo huyu mchafu. "Anapotoka, hupitia mahali pasipo na maji, akitafuta mahali pa kutulia." Biblia ilisema, "Hangeweza kupapata, hivyo basi anasema, 'Nitarudi nilimotoka.'" Anarudi kwa mtu huyu ambaye wakati mmoja alikuwa ndani yake, naye anakuta nyumba imefagiliwa vizuri, imesafishwa, imetakaswa, hukumu yote imetoweka. Loo,

mwaminio mwenye furaha tu, lakini ni mtupu. "Naye akasema, 'Njoni hapa,' pepo wengine saba waovu kuliko vile yeye alivyokuwa." Je, mtajaribu kupata hili tafadhalini? Biblia ilisema hiyo ni Kweli. Yesu alisema ni Kweli. "Basi anarudi kwenye nyumba hii."

60 Mtu ambaye amemkiri Kristo kuwa Mwokozi wake, ameacha uovu wake, ameacha ulevi wake, ameacha sigara zake, uongo wake, wizi wake. Ametakaswa, amesafishwa. Nyumba yake yote imefagiliwa. Anajisikia huru. "Kwa hiyo anarudi na kuipata nyumba hiyo. Ndipo anaenda na kuwachukua pepo wengine saba waovu kuliko alivyokuwa, na kumwingia mtu huyu." Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Hali ya mwisho ya mtu huyo ni mbaya mara saba kuliko ilivyokuwa hapo kwanza."

61 Sasa nini kimetokea hivi punde? Mwinjilisti anapita, wanahubiri toba, nawe unasafishwa dhambi yako. Ndipo basi unaposafishwa, ibilisi anakuondokea. Unarudisha vitu vyako, ambavyo uliiba. Unaenda, ukakiri makosa yako kwa mkeo au mumeo. Unajisafisha kabisa. Ndipo basi, jambo ni kwamba, wewe ni safi tu, na umefanywa shabaha nzuri sana ya ibilisi.

62 Sasa, "Baada ya watu kuamini na kubatizwa, walijazwa na Roho Mtakatifu." Na huo ndio mpango wa Kiungu wa Mungu. Sasa, ikiwa umejazwa na ulimwengu. . .Basi unapookoka, huenda ukajazwa na mawazo mazuri, na kadhalika; lakini isipokuwa umejazwa na Mungu! Mungu alimtuma Roho Mtakatifu, duniani, ili kulihamasisha Kanisa.

63 Nawe unaweza kujazwa na mawazo. Unaweza kujazwa na theolojia. Na unaweza kujazwa na elimu, ujuaji. Na unaweza kujazwa na dini, na bado ukawa shabaha ya ibilisi. Hiyo ni kweli. Sasa, wakati . . .

64 Mungu alikuumba ili uweze kujifanya mtupu. Kwa maana, ulipozaliwa, uliumbwa ukiwa na mahali pa kujazwa. Kwa asili, wewe ni mtoto wa ibilisi. Na wakati wewe. . .Mwinjilisti anapokuja, nawe unatubu na kusafishwa.

65 Unaona nini? Ibilisi anakuja. Anakurudishia, na kukuweka katika dhehebu fulani dogo, na kusema, "Kanisa letu ndilo kubwa zaidi." Umekosea, papo hapo, kwanza kabisa. Kisha unakuwa mkaidi, mwenye kujivuna. "Mbona, hainihukumu kukaa nyumbani na kutazama televisheni. Hainihukumu kuvuta sigara kidogo ya kirafiki au kunywa pombe, mara moja moja." Matunda yako yanaonyesha kile ulicho.

66 Halafu utamsikia kasisi mmoja akiinuka. Na huenda ikawa unasoma Biblia, nawe unaona mahali ambapo Yesu alifanya na kutenda miujiza. Unampelekea mchungaji. "Loo," atasema, "sasa, angalia. Hatuamini Hilo." Hao "sisi" ni akina nani? Ni nani "*sisi* hatuamini Hilo"; yeye na nani? Si yeye na Mungu, kwa maana Mungu ndiye aliyeliandika. Ni yeye na mtu mwingine.

67 Na ikiwa utalifuatilia, ni nia ile ile iliyokuwa kwenye mnara wa Babeli, kujenga utawala wa kidunia wa kujibunia. Lakini Mungu hataki hilo. Hataki ninyi nyote muungane chini ya Methodisti, chini ya Baptisti, ama chini ya . . . uongozi wowote wa kikanisa, wa kanisa. Hataki ninyi nyote muungane chini ya Rumi. Hataki ninyi nyote muungane chini ya . . . mamlaka yoyote ya kanisa.

68 Anataka muungane chini ya Ufalme Wake wa kiroho, Roho Mtakatifu. Ndipo Roho Mtakatifu ajapo, ulimwengu unakufa, nanyi mnajazwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Naye ibilisi ni mtu anayepaswa kukaa mbali na wewe. Uko chini ya milki ya Mungu. Wewe ni kiumbe kipya. Roho Mtakatifu anaingia mahali hapo patupu na kupajaza.

69 Sasa, mchungaji, dhehebu lolote, fasihi kidogo ambayo ungesoma, inaweza kukwambia, “Siku za miujiza zimepita.” Hapo ni mahali pazuri kwa ibilisi kupenyeza mojawapo ya hao pepo hapo ndani na kukufanya mtu mvovu kuliko ulivyokuwa wakati ulipokuwa mwenye dhambi. Maana, mwenye dhambi wa kidini ndiye mbaya kuliko wote. Huyo ndiye mbaya zaidi. Yesu alisema hivyo. Ndiye pepo mwovu kuliko wote.

70 Halafu unaweza kwenda kwenye mkutano ambapo nguvu kuu za Bwana! Na jambo la kwanza ungesema, ulipoziona, “Sasa, nashangaa tu. Nikijihusisha na Hili, watanipa barua yangu kanisani.” Unaona ulipo?

71 Sasa, labda sivyo. Kuna madhehebu mazuri, wachungaji wazuri, Wamethodisti, Wabaptisti, aina zote tofauti wanaoamini katika matendo ya kimbinguni ya Mungu, wanaoamini ya kwamba mwanadamu hana budi kuzaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu. Nami namshukuru Mungu kwa kila mmoja wao. Wapo wengi wao wanaoamini. Mungu anao watoto Wake waliokwamia kila mahali. Lakini ninachojaribu kusema, katika wingi mnaona, makanisa hayo yote.

72 Ninataka kuwauliza ninyi Wamethodisti jambo fulani, msioamini katika uponyaji wa Kiungu. Vipi kuhusu John Wesley, mwanzilishi wenu? Alipokuwa amempanda farasi wake, akamwombee mwanamke mgonjwa, naye farasi akajikwaa katika shimo la fuko, akaanguka na kuvunja mguu wake. John akashuka kwenye farasi wake, akachukua chupa ya mafuta, na kusema, “Bwana, umemwumba farasi huyu, kama vile ulivyoniumba mimi,” kisha akampaka huyo farasi mafuta. Akampanda na kwenda zake. Vipi kuhusu hilo? Ukiuhubiri katika kanisa la kisasa la Methodisti leo, wangekutupa nje ya mlango. Hakika.

73 Lakini mnaona ni kitu gani? “Yule mama kahaba wa kale,” wa Biblia, Ufunuo 17, alikuwa na binti. Na hakika sihitaji kuingilia hilo kwa undani. Uprotestanti ni mzao wa Ukatoliki. Bila shaka, ndivyo ulivyo. Walitoa vitu vyao vingi

sana, wangali wanavishikilia. Wangali wanafanya hivyo, mbali sana na Mafundisho ya Maandiko, mbali kabisa na Mafundisho ya Mitume.

74 Walijitengenezea Kanuni ya Imani ya Mitume. Ninataka mtu yeyote aniambie ni wapi mitume waliwahi ku—kunukuu kanuni ya imani kama hiyo. Hasha, hasha! Lakini ninyi mnalishikilia.

75 Nanyi mnawaita makasisi wenu, "Baba." Naye Yesu alisema, "Usimwite mtu 'Baba.'"

76 Nanyi watu, mnatoa vitabu vyenu vidogo vya maombi, Waprotestanti na Wakatoliki pia, na kukariri maombi, tena na tena na tena, Protestanti na Katoliki pia. Naye Yesu alisema, "Usitumie marudio ya bure kama wapagani wafanyavyo; wanadhani wanaweza kusikika, kwa mazungumzo yao mengi."

77 Unaona, sufuria haiwezi kusema birika ni nyeusi. Hiyo ni kweli. Zote ziko chini ya hukumu, kila nadharia ya kujibunia. Na hiyo ndiyo sababu katika uamsho kama huu, unapokuja mjini, viti hivi ni vitupu. Lakini Mungu atalituma, hata hivyo, na magazeti yatalieneza. Na kwenye Siku ya Hukumu, utakapoitwa kujibu, utapatikana na hatia kama walivyopatikana nayo huko nyuma.

78 Hivi Yesu hakusema, "Malkia wa Sheba, Malkia wa Kusini, alikuja kutoka sehemu za mbali zaidi za dunia," ameketi juu ya mgongo wa ngamia, miezi mitatu, "kuona karama ya Mungu, ambayo ilikuwa ni Sulemani"? Akasema, "Amin, nawaambia, aliye mkuu kuliko Sulemani yuko hapa."

79 Nami ninasema, usiku wa leo, ya kwamba aliye mkuu kuliko Sulemani yuko hapa. Ni Utu wa Kristo, katika Roho Mtakatifu, ukitenda na kufanya kazi, ukizalisha katika maisha ya mwanadamu kama tu alivyofanya hapa.

80 Mungu alikutengenezea mahali panapoweza kufanywa tupu. Sasa, huwezi tu kuyang'arisha maisha ya kale. Huwezi kuyakarabati maisha ya zamani. Hayana budi kufa, ndipo maisha mapya yazaliwe ndani yake. Hahitaji rangi ya makucha ama ni kitu gani mnachopaka midomoni mwenu, kile ambacho wanawake hufanya, mwajua, kuwafanya waonekane bora zaidi. Yeye hahitaji vikoleo vya nywele. Hahitaji vitu vya mdomo. Kanisa linahitaji Kuzaliwa na kujazwa na Roho Mtakatifu.

81 Huku amezikunja nywele na midomo yake kupakwa rangi, bado ni maskini msichana yule yule wa kale. Bado ana shaka. Angali hivyo, ana mashaka yake. Ana hofu zake. Amevurugika kabisa. Wala hataki kusikia Kweli, kwa maana kitu kilicho ndani yake hakitamruhusu kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Bila shaka.

82 Mwanamke mwenye sifa mbaya mitaani, ukimwendea na kumwambia, "Aise, mwanamke, umekosea."

Atasema, "Shika lako."

83 Basi mfuasi fulani wa kanisa mwenye shingo ngumu ni mwovu mara saba kuliko mwanamke huyo.

84 Mwambie, “Kuna uamsho mkubwa unaoendelea. Unapaswa kuja. Bwana Yesu amejidhihirisha Mwenyewe, akiwaponya wagonjwa. Watu wananinii, kadhalika, wanampokea Roho Mtakatifu.”

85 “Endelea! Una shida gani? Mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni mzuri kama ulivyo wewe.” Kwa nini? Yeye hajui vizuri zaidi.

86 Lakini hebu zungumza na mwanamke mwadilifu na kumwambia ni kosa kufanya hivyo. Atasema, “Amina. Najua hilo ni kosa.”

87 Hebu mwambie mwanamume au mwanamke, ambaye amezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu uko hapa kwa ajili yao, kuijaza mioyo yao. Watapaza sauti “amina” Kwake, kwa maana wao hula na kuishi kwa Neno la Mungu. Bila shaka, wanafanya hivyo.

88 Lakini, mnaona, kama ilivyo ulimwenguni ndivyo ilivyo kanisani. Wanajaribu kujenga kitu fulani. Mungu hahitaji msaada wako kuujenga Ufalme Wake. Mungu anakutaka tu ulihubiri Neno. Yeye atajenga jengo. Yeye ndiye Msanifu mijengo. Ana ramani zimewekwa Hapa. Vema.

89 Tufanye nini basi? Mungu alikufanyia mahali pa kujifanya tupu, kwa mambo ya ulimwengu. Sasa, maumbile yaliweka roho mle ndani inayokufanya uyapende mambo ya ulimwengu, nawe unajua umekosea unapofanya hivyo.

90 Hata kama wewe ni mshiriki wa kanisa, unaweza kuwa wa kidini tu uwezavyo kuwa, huku umejaa ibilisi kabisa, nayo. Hiyo ni kweli. Kama unatilia shaka Neno la Mungu, kila Neno Lake kuwa ni kweli, ni ibilisi anayekuambia hilo. Bila shaka, ndivyo ilivyo. Huo ni ujuvi. Lakini ni wakati, wakati umefika ambapo maskini mhubiri fulani dondoadume atavua glavu zake na kuhubiri Injili jinsi ilivyoandikwa, na kuacha kujaribu kujipumbaza na ujuzi wa seminari.

91 Siku zote nilimhurumia kuku wa kiangulio. Kuku aliyezaliwa ndani ya kiangulio, hulia, wala hana mama wa kumwendea. Hilo linanikumbusha juu ya mhubiri wa seminari ambaye hajui zaidi kuhusu Neno la Mungu kuliko vile seminari ilisema; akilia, wala hana Mama wa kumwendea.

92 Lakini unapozaliwa kweli chini ya mbawa za neema na nguvu Zake, utakubaliana na kila Neno alilosema Yeye, ni Kweli. Ndipo Mungu anaposonga mbele katika mambo ya kimbinguni, moyo wako utakuwa na njaa moja kwa moja Kwake.

93 Hutaenda kando na kusema, “Telepathia ya akili! Ibilisi! Beelzebuli! Siamini Hilo. Kanisa langu halifundishi Hilo.”

94 Utasema, “Mungu asifiwe milele,” kwa kuwa umejazwa. Huwezi kukaa tupu.

95 Tupu ni uvivu. Hiyo ndiyo shida ya waongofu siku hizi. Mara tu unapoongoka, unaanza kuzembea. Unapaswa kuwa pale magotini mwako, ukitafuta Mungu kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, upate kujazwa. Ndipo una ukuta, Uwepo Wake uliobarikiwa pamoja nawe. Ndipo adui anapoingia, kama simba katika lile tundu usiku ule pamoja na Danieli, Nuru ya Mungu inang'aa naye anakuondokea. "Kama mwenye nyumba hajaizingira." Bila shaka.

Sasa, tumeungana, kwenye Siku ya Pentekoste.

96 Au, kabla tu yake, wanafunzi wote walikuwa wamesafishwa, dhambi zao zote zilikuwa zimesamehewa. Naye Yesu, Mchungaji, maskini yule kuku, tuseme, kama vile Yeye alivyosema "angewakusanya kama kuku," vifaranga Wake. Ndipo, wakati roho ya ibilisi ilipozuiliwa, wakingojea wakati wa kujazwa.

97 Na, hata hivyo, katika hayo yote, watu kumi na wawili tu, mmoja wao alipata upako wa ibilisi, na baada ya kumwona Yesu akifanya kazi hizo zote nzuri. Yeye ndiye aliyewaongoza askari kumfunga kitambaa kichwani, na kumpiga kichwani kwa rungu au fimbo, na kusema, "Tuambie ni nani aliyekupiga. Tutakwamini." Baada ya kumfuata Yesu na kuona miujiza yake, na kusikia. Yule Myahudi akaja, ndipo Yesu akamwambia yeye alikuwa ni nani, alikotoka. Baada ya kuona hayo yote, mtu yuyu huyu alilitilia shaka, baada ya kumwona kwenye kisima cha Samaria, pamoja na yule mwanamke, akamwambia dhambi zake. Na kumsikia yule Farisayo akisema, "Yeye ni mpiga ramli." Na kisha baada ya kumwona Yesu mpendwa, yule mwanamke akigusa vazi Lake na kuponywa, bado asingeweza kuamini. Ndipo akaruhusu pepo wa kutoamini amjie kwa sababu alikuwa amefundishwa kwa nje. Mnaona ninachomaanisha?

98 Loo, kutokuamini ni jambo la kutisha jinsi gani! Na hata hivyo, watu wanaokiri Ukristo, wakiketi na hilo ndani yao. "Wakaidi, wenye kujivuna," Biblia ilisema, "katika siku ya mwisho." Je, ninajisikia kigeni kuhusu hilo? Hapana, bwana. Linanifanya kujua hili, ya kwamba wakati wa mwisho umekaribia. Kwa maana Biblia ilisema, "Roho anena waziwazi," unajua neno *waziwazi* lina maana gani, "kwamba katika siku za mwisho," ndizo hizi, "nyakati za hatari zitakuja, kwa maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe."

99 "Mimi ni Dkt. Ph.D. Jones, na ujuzi wa—wangu wa seminari. Ni—nina digrii zangu zote. Mimi ni LL, L maradufu, D. Mchungaji wetu ni vyote *hivi, vile*." Hilo halina uhusiano wowote na Mungu.

100 Nilikuwa na mtu aliyekuja, si muda mrefu uliopita, akasema, "Ndugu Branham, ninaweza kuukandika ukuta wako kwa digrii." Kisha akasema, "Kila wakati, nilipopata shahada yangu ya udaktari, nilifikiri ningempata Kristo. Nilipopata

shahada yangu ya fasihi, nilipopata shahada yangu ya kwanza, nilimwinda Kristo katika hayo yote. Na bado sijampata." Akasema, "Je, waalimu wamekosea?"

101 Nikasema, "Kristo hajulikani kwa digrii hizi za kitheolojia, bali Yeye anajulikana katika utu wa Roho Mtakatifu aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste."

102 Ndipo mtu huyo akaanguka kwenye meza yangu ya kahawa, kwenye chumba changu cha kulia chakula, na hapo akampokea Roho Mtakatifu. Amina. Uwanjani usiku wa leo, akihubiri uponyaji wa Kiungu, ambaye ni mmoja wa watu mashuhuri wa siku hizi. Kanisa lilifanya nini? Likamfukuza, upesi sana. "Heri ninyi watakapowatoa katika masinagogi na kadhalika, kwa ajili ya Jina Langu."

103 Kile Biblia ilisema, "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna." Lini? "Katika siku za mwisho. Wapenda televisheni, anasa, kuliko kumpenda Mungu. Wasiopenda kufanya suluhu, wasingiziaji."

104 "Sasa nitakwambia. Usishuke kwenye mkutano huo, kwa sababu hakuna kitu kwake." Wasingiziaji! Biblia ilisema hivyo. "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake." Nguvu gani hizo?

105 Wanafunzi waliuliza. Hebu kidogo. Wanafunzi waliuliza swali hili walipoona ya kwamba Yuda alikuwa amemsaliti na kila kitu kilikuwa kimekaribia. Walisema, "Bwana, wakati huu utawarudishia Israeli ufalme?" Angalieni kile Yeye alisema. "Sio kazi yenu kujua majira hayo. Lakini pandeni hadi kwenye mji wa Yerusalemu, nanyi mtavikwa uwezo utokao Juu kabla hamjaweza kuwa shahidi." Shahidi hana budi kujua kitu fulani. Shahidi hana budi kuwa na ujuzi. Wala huwezi kuwa shahidi wa Kristo mpaka Roho Mtakatifu amekubatiza.

106 Yesu hangewaruhusu wanafunzi Wake kuhubiri Injili mpaka walipompokea Roho Mtakatifu. Hata hivyo, walikuwa wamepewa heshima ya kutembea pamoja Naye, miaka mitatu na nusu. Ingawa walikuwa watu watakatifu, waliokubalika machoni Pake, lakini Yeye hakuwaacha waende kuhubiri mpaka walipongoja kule juu na kujiondolea tofauti zote, ndipo Roho Mtakatifu akaja.

107 Kile ambacho ulimwengu unahitaji siku hizi ni ujazo uo huo. Kufanywa tupu kunapokuja, kujazwa kunahitajika. Ujazo huo hufanya nini unapoingia? Mahali ulipo na shaka, huleta imani. Mahali ulipo na kutokujali, huleta upendo. Mahali ulipokuwa na chuki, huleta ushirika.

108 Na halafu, wakati, Kanisa la Mungu aliye hai siku moja litaunganishwa chini ya Kichwa kimoja kikuu, na hicho kitakuwa ni—ni Kichwa cha Mungu. Mungu, na katika umoja wa Mwili wa Kristo, atakuwa Gavana na Mfalme na Bwana, juu ya Kanisa zima, chini ya udhibiti Wake. Kisha litapokelewa juu.

109 Siku hizi, minara yote ya Babeli wanayoweza kujenga, roketi zote wanazoweza kupata, ujamaa wote na ukomunisti wote wanaoweza kuchochea, mifumo yote ya kikanisa itashindwa. Lakini licha ya hayo yote, Mungu atakuwa na Kanisa lililounganishwa chini ya Mfalme Wake, chini ya Ufalme Wake, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

110 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka au kunywa kitu chochote cha kufisha, hakitawadhuru. Wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Ishara kuu na maajabu! "Kazi nizifanyazo Mimi wao nao watazifanya. Hata zaidi ya hizi watazifanya, kwa maana Mimi ninaenda kwa Baba. Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi." Ati nini? Tupa nje, jifanye tupu. "Kisha nitakuwa ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu, utimilifu." Bila shaka. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu."

111 Wakati huyo Roho yuko mle ndani, Yeye hushika Neno la Milele la Mungu, Naye huita kila kitu kinyume Chake kana kwamba hakikuwepo, haidhuru nini kinachotukia, yale ulimwengu usemayo, yale chochote kile kinasema. Ikiwa Mungu ametoa ahadi, mtu ambaye amevikwa Roho huyo atashikilia ahadi hiyo ya Mungu, kwa sababu hakuna kitu kingine njiani mwake.

112 Kanisa ni safi. Kanisa husafishwa na Roho Mtakatifu. Dhamiri zao, hofu za shaka na kutokuamini zinaondolewa. Ndipo wanaposikia Neno la Mungu likisema jambo fulani, wanaliamini. Loo! Wanalishikilia. Kamwe hawaliachilii.

113 Nao ulimwengu siku hizi, rafiki yangu, unataka kuwaona watu ambao wameunganishwa na Kristo, kuonyesha Roho halisi wa Kristo. Mashujaa hodari!

114 Katika kumalizia, naweza kusema, ulimwengu unataka kuona mashujaa. Wanamheshimu shujaa. Hilo ni zuri. Ule msemo wa kale ni kwamba, "Waoga hufa mara milioni moja, wakati mashujaa hawafi kamwe."

115 Kuna hadithi inayokuja niani mwangu. Ningependa kuwanukulia kwa muda mfupi tu. Ni hadithi ya shujaa ambaye mara nyingi sana husahaulika. Wengi wenu ninyi wanaume, wa rika yangu, nanyi wanawake, mtaikumbuka vizuri katika vitabu vyetu vya shule.

116 Ilikuwa miaka mingi iliyopita, huko Uswisi. Maskini wale Waswisi walikuwa wamepanda milimani na kujijengea nyumba kadhaa. Walikuwa na uchumi wao mdogo, na kadhalika, nyumba zao ndogo. Nao walizipenda. Hawakuwa watu wa vita. Walikuwa watu wenye amani.

117 Na mara ghafla, wakati mmoja, likija Uswisi, lilikuwa ni jeshi kubwa lenye nguvu. Nao walikuwa watu waliofunzwa

vizuri, wamejipanga tu kama viti hivyo hapo, kama tu ukuta wa matofali; ngao kubwa, mikuki mikubwa, watu wa vita waliofunzwa vyema. Nao wakaja taratibu wakiingia Uswisi, kunyakua mali ya Waswisi.

118 Nao Waswisi, ili kulinda nyumba zao, waliwaaga wake zao kwa busu, na watoto wao wakubwa na wachanga, walichukua vipande vya kale vya panga, miamba na mawe, marungu makubwa mno ya kale, kisha wakashuka bondeni, kukutana na jeshi linalokuja. Ndipo walipokusanyika pale, kundi dogo tu la watu, huku wamezingirwa na jeshi kubwa linalotembea taratibu. Wangeweza kufanya nini? Walisimama bila matumaini, bila uwezo, mmoja akimtazama mwenzake. Walikuwa wameshindwa kabisa. Hakuna njia ya kuepukia. Walikuwa wamekwisha.

119 Baada ya kitambo kidogo, kulikuwako na mtu mmoja jina lake Arnold von Winkelried. Akajitokeza, naye akasema, "Enyi watu wa Uswisi, huko ng'ambo ya mlima kuna nyumba ndogo nyeupe ambamo mke wangu na watoto watatu wadogo wanangoja." Kasema, "Nilipowaaga, asubuhi ya leo, sitawaona tena katika dunia hii."

120 Wakasema, "Arnold von Winkelried, utafanya nini?"

Akasema, "Leo hii, nitaifia Uswisi."

121 "Vema," wakasema, "Arnold von Winkelried, hilo halitasaidia chochote. Kwa nini unasema utakufa kwa ajili ya Uswisi?"

122 Akasema, "Ninyi chukueni mlicho nacho; majembe, maskini miundu ya kale, fimbo na marungu, mawe." Kasema, "Nifuateni, na mpigane vizuri mwezavyo kwa vile mlivyo navyo."

Kasema, "Kwani utafanya nini?"

123 Ndipo akatupa chini mundu wake, kitu chake alichokuwa anaenda kupiga vita nacho. Akainua mikono yake juu, na kulipigia kelele jeshi hilo kubwa.

124 Akatazama pande zote. Akaona mahali palipokuwa na mikuki iliyokuwa imeshikana sana. Kila mtu amevaa nguo rasmi, akitembea taratibu moja kwa moja kuukabili mlima, mbele, mbele. (Loo, hivyo ndivyo ibilisi anavyofanya.) Akiwasukumia moja kwa moja pembeni.

125 Akainua mkono wake, akapiga makelele, "Simile uhuru upatikane!" Ndipo hilo jeshi linalokuja likashangaa kuna nini. Ndipo akaanza kukimbia, kisha akapiga makelele tena, "Simile uhuru upatikane!"

126 Ndipo alipoingia moja kwa moja kwenye lundo hili kubwa la mikuki, ambako mingi ilielekezwa, kumnasa, akainyosha mikono yake *hivi*, na kukamata mikuki mingi mikononi na kuichomelea kifuani mwake. Onyesho kama hilo la ushujaa wa kweli, lililivuruga jeshi hilo kubwa, na kulishinda kabisa.

127 Hawa hapa Waswisi wakaja, na marungu na fimbo, na kulipiga jeshi hilo na kulifukuza kutoka katika taifa lao. Wala hawajawahi kuwa na vita tangu wakati huo hata sasa, kwa sababu mtu mmoja alifanya kazi ya shujaa na akafanya yaliyo mema. Hiyo haijawahi kupitwa, na hulinganishwa kwa nadra sana, kama ushujaa.

128 Lakini, loo, hilo ni jambo dogo sana, ukilinganisha na siku moja, miaka mingi iliyopita, wakati watoto wa Adamu, jamii ya ulimwengu huu, ilipofinyiliwa pembeni, kwa maradhi na magonjwa na dhambi. Walikuwa wametumiwa manabii, nao wakawaua. Nao, kila aina ya torati, na kuzikataa. Nayo jamii ya Adamu ilikuwa imefinyiliwa kwenye kona.

129 Kulikuwa na Mtu aliyetoka Mbinguni, na kusema, "Ninashuka kwenda duniani leo hii kuyatoa Maisha Yangu." Akapata mahali palipokuwa na mishale mingi zaidi. Nayo hofu ya jamii ya Adamu ilikuwa ni mauti. Akanyakua mauti, alipoenda Kalvari, na kuyavuta akayaingiza kifuani Mwake.

130 Naye akawaambia wanafunzi Wake, "Jifanyeni tupu sasa. Nendeni huko kwenye. . .Ngojeni kule mpaka niwatumie tena Kitu cha kupiga nacho vita." Libarikiwe. . .Samahani. Jina la Bwana libarikiwe. Akamtuma Roho Mtakatifu, na kusema, "Nifuateni. Katilieni mbali dhambi na magonjwa hata ukutani."

131 Wanaume na wanawake, jambo kuu zaidi ambalo limewahi kupewa Kanisa la Mungu si kushika karatasi fulani ya kikanisa mkononi mwako, bali kujazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, na kuukata ufalme wa ibilisi hata Jemadari wetu Mkuu atakapokuja kuchukua mamlaka.

132 Mungu awabariki. Msifikiri nimerukwa na akili. Hiyo ni kweli. Najua ninachozungumzia. Wanaume wa heshima; wanawake, wewe unayemwamini Mungu; wewe unayedai kuwa na Roho wa Mungu moyoni mwako. Ikiwa wewe ni mgonjwa au mhitaji, unayo silaha hapo ya kupigana na ugonjwa huo. Iko ndani yako. Mungu alikupa wewe.

133 Kwa nini tusimame nyuma kama mwoga? Kwa nini tusimame kando? Hebu tumfuate Jemadari. Hebu tumfuate Yeye aliyeenda Kalvari. Alipoenda Kalvari, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

134 Chukua kile akupacho, na upigane na magonjwa na dhambi. Pambana na kutokuamini. Mwambie ibilisi yeye ni mwongo. Kristo alisema ameushinda ulimwengu. "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu." Nguvu za Kristo ni kuu, ndani yenu, kuliko huo ugonjwa ulio nao mwilini mwako usiku wa leo. Nguvu za Kristo ni kuu kuliko ile dhambi ndogo, inayotuzinga ambayo huwezi kuishinda. Hebu na tumchukue huyo Roho Mtakatifu na tupambane na Ibilisi kabisa, na tutoke tukiwa washindi, kama mashujaa wa msalaba.

Na tuombe.

135 Yehova, Yehova-rafa, Yehova-yire, tunakuja katika Jina la Yesu. Tunakuja kwa sababu Yeye alisema, “Mwombeni Baba neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya.”

136 Hili hapa kundi dogo la watu hapa, usiku wa leo, ambao wanayumbayumba, wakijaribu kukaa chini ya bendera, naye ibilisi anawazomea. Wanatazama kule nje kwenye jeshi lile kubwa lililo kama ukuta ambalo limewazingira, na kuwaambia, “Siku za miujiza zimepita, na hakuna kitu kama hicho.”

137 Ee Bwana Mungu, jalia washike kwa dhati huo Uzima wa Milele ambao umeijaza mioyo yao, Roho Mtakatifu. Na kama hajawajaza, jalia afanye hivyo sasa hivi. Jalia mashaka yote yatoweke. Na jalia kundi hili dogo la watu, usiku wa leo, lijazwe na nguvu za Mungu za kujaza, kuchukua mahali pa kutokuamini na kutilia shaka. Na uwape imani, na upendo, na furaha, na shangwe, na Roho Mtakatifu, kushikilia ahadi hiyo ambayo Mungu alitoa, kama Ibrahimu wa kale, na kuviita vitu ambavyo haviko kana kwamba vilikuwako, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Tujalie, Bwana.

138 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, kila mahali katika jengo hili, sijui kama kunaweza kuwa na mtu hapa asiye na Roho Mtakatifu, usiku wa leo, angesema, “Ee Bwana, unirehemu. Ninaona aibu kwamba ninazembea kwenye minara hii ya mifumo ya kujibunia ya kikanisa ya mashaka haya yote na kadhalika wanayotoa kwake. Bwana, nitoe katika utawala huu, usiku wa leo, na uniweke katika utawala Wako, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninautaka sasa, Bwana. Nipe imani ya kuamini kwa ajili ya uponyaji wangu. Nipe imani kuamini dhambi zangu zimetoweka, na mambo haya yote. Nipe imani ili Roho Mtakatifu aingie ndani yangu na kuilowesha nafsi yangu kwa shangwe.” Je, unaweza kumwinulia mikono yako na kusema, “Ninataka kumpokea”?

139 Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Kote jengoni. Mungu akubariki huko nyuma, mama. Nasubiri. Mungu anaangalia. Na wewe hapa, safu hii yote hapa ndani. Naam. Mungu akubariki.

140 “Nataka Roho Mtakatifu. Nimechoka, nikizunguka, maisha nusunusu. Hasira, na mizozo na hamaki, na mashaka na hofu vyote viko moyoni mwangu, Ndugu Branham, bali nataka vyote vitoke. Ninataka kuwa mahali ambapo ninaweza kuwa nuru inayoangaza. Ninataka niwe, maisha yangu, niwe kama Stefano, jinsi alivyokuwa bila woga.”

141 Walisema uso wake uling’aa kama malaika. Sio lazima awe na mng’ao mkali. Malaika angekuwa mkali. Alijua alichokuwa akizungumzia. Alisimama mbele ya lile Baraza la Wazee na kusema, “Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa, mioyo na masikio! Mnampinga Roho Mtakatifu. Kama baba zenu

walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo." Alikuwa malaika. Alikuwa na ujumbe. Neno *malaika* linamaanisha "mjumbe."

142 "Nipe, nifanye mjumbe, Bwana, wa nguvu za Kiungu za Kristo, kwa Roho Mtakatifu moyoni mwangu." Je, unaweza kuinua mkono wako, mtu mwingine ambaye hajainua?

143 Baraka juu yako, bwana. Baraka juu yako, msichana. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Bwana anakuona. Vema. Sawa.

144 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, hebu na tuombe Mungu awajaze na Roho Mtakatifu, papo hapo mlipo.

145 "Ndugu Branham, unataka kushuka, uniwekee mikono yako, kwa ajili ya Roho Mtakatifu?" Sio lazima.

146 "Petro alipokuwa akisema Maneno haya katika nyumba ya Kornelio, Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia Neno." "Imani chanzo chake ni kusikia," sio kuwekewa mikono, bali kwa kusikia, "kusikia (nini?) Neno la Mungu."

147 Nimejaribu, kwa njia yangu nyenyekevu, kuwaonyesha minara inayojengwa, minara ya Babeli ambayo haina budi kuanguka. Nami ninawaelekeza kwenye Mnara. Na kuna njia moja tu ya kupanda Kule, hiyo ni kupitia kwa Roho Mtakatifu.

148 Huwezi kukaa bila kuegemea upande wowote. Biblia ilisema, katika siku hizi, kwamba, "Kila mtu ambaye hakutiwa muhuri na Roho Mtakatifu angekuwa na alama ya mnyama." Alama ya mnyama ni nini? Kutokuamini. Hamjui ni nini... ikiwa wachungaji wenu wamewafundisha. Katika Agano la Kale, wakati baragumu ilipolia, kama huyo mtu alitaka kuwa huru, angeweza kuwa huru. Ikiwa hakutaka, angeenda kwenye mwimo na kutobolewa sikio lake kwa uma, kwa sababu alikataa kuwa huru. Basi ukikataa kuwa huru, basi utamtumikia mnyapara huyo siku zako zote, nawe umepotea.

149 "Muhuri wa Mungu ni nini, Ndugu Branham?" Roho Mtakatifu.

Unasema, "Je, hilo ni la Kimaandiko?" Kabisa, mengi.

150 Hebu niwape moja ili msilisahau. Waefeso 4:30 ilisema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Huo hapo Muhuri wa Mungu. Hicho ndicho ninachojaribu kuwaambia. Mmeutazamia Muhuri wa Mungu kuja katika siku za mwisho. Hauko kwenye paji la uso wako. Kusema ulikuwa kwenye *paji la uso* wako ni "maarifa, kuelewa" kwako. Lakini Biblia ilisema Muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na kila mtu aliye Nao, mioyo yao iko huru. Wametiwa muhuri kwa maarifa ya Mungu, katika vipaji vya nyuso zao, kwamba wanajua kwamba Yesu amekufa na akafufuka tena, kwa sababu wanaweza kumwona.

151 "Bado kitambo kidogo, na asiyeamini hataniona tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona," wale walio na ule Muhuri, "kwa kuwa

nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu. Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, hata kubwa kuliko hizi, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu."

152 Ulimwengu usioamini unatembea katika giza zito, kuzunguka mnara fulani wa Babeli. Mguso, na wana kitu kimoja ama kingine kwenye ushirikina fulani, dhehebu fulani. Wakati, mwaminio halisi ana ishara na maajabu, nayo yamefichwa kutoka kwenye macho ya asiyeamini. Fungueni mioyo yenu sasa na mumruhusu aingie.

153 Nitawauliza wahudumu, pia, humu jengoni, kuomba hasa kwenye wakati huu.

154 Huu ni wakati muhimu sana. Wakati huu utatia muhuri kikomo, hapana shaka, cha wengi. Nafsi moja ina thamani ya dunia elfu kumi! Jinsi wakati huu ulivyo mkuu.

155 Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Yehova, nyosha mkono sasa hivi kwa rehema za Bwana Yesu, Yule Mbarikiwa, na umimine Mafuta Matakatifu ya Roho Wako katika kila moyo hapa, wale walio na njaa. Imeandikwa katika Biblia, "Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Si ajabu; wote walikuwa na kiu. Wewe ulisema, "Heri ninyi mnapokuwa na njaa na kiu ya haki, kwa maana mtashibishwa."

156 Je, tunawezaje kuzungumza na watu kuhusu Kristo wakati hawamwonei Yeye kiu? Wakati, wameketi katika mawazo yao ya kujibunia, na kuridhika, bila kujua kwamba wao ni "wenye mashaka, wanyonge, vipofu, na maskini, wala hawajui."

157 Mungu, uturehemu, usiku wa leo, kwa wale wanaoinua mikono yao, wale ambao wako tayari kwa Roho Mtakatifu kuingia. Jalia aje, ashuke kwenye vijito vya baraka Zake sasa, akimiminika katika kila moyo, na kuwajaza kwa furaha tele, ili wapate kujua ya kwamba Yeye yu hai. Wape ufahamu wa jinsi ya kukukubali Wewe. Wape ufahamu ya kwamba Wewe upo, ukipenda sana kuingia mioyoni mwao kuliko wao wanavyotaka kukupata Wewe.

158 Jalia kila hisia ndogo ya kigeni, kila pepo anayeketi karibu, akizomea, "Sasa, hutaupokea. Hutaupokea." Jalia wamwite ibilisi huyo "mwongo." Mungu alitoa ahadi, na Mungu atatimiza ahadi Yake. Lakini tunawezaje, wakati tunaketi sote tumejivuta ndani kama kasa kwenye ganda lake?

159 Ninaomba, Mungu, ya kwamba utafungua umati huu wa watu, na kumshusha Roho Mtakatifu kutoka huko Juu, kwa mshindo mkuu wenye nguvu juu yao. Mioyo yao na iwe wazi sasa. Na kama wanaweza tu kumpokea Roho Mtakatifu, Bwana, Yeye atawatangazia ya kwamba baraka zote za Mungu ni zao. Tujalie, Baba, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

160 Je, hamumpendi? Mnaamini ya kwamba Hii ni Kweli? Mimi si mhubiri sana wa kikanisa. Mimi . . . Lakini kile mimi . . .

161 Laiti ningeweza tu kuelezea kile ninachokiona moyoni mwangu! Ninauona wakati wa mwisho. Najua huu Ujumbe ni wa kweli. Kama nilikuwa nikifa saa hii, huu Ujumbe ni wa kweli. Mnaona? Nami ninaamini ya kwamba macho ya watu, mara nyingi, yamepofushwa. Lakini, Mungu ni mwenye haki, katika kila wakati. Alimtuma Nuhu. Ni wangapi waliookolewa? Ni wangapi waliookolewa katika siku za Lutu? Yesu alisema, "Ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Bila shaka, mnaona, wachache tu. Lakini Ujumbe uliendelea, vivyo hivyo tu.

162 Sasa sikilizeni. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu yuko hapa? Hebu tuone mkono wako. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye ni *Yehova-Rafa*, "dhabihu ya Bwana iliyotolewa"? Ni wangapi wanaoamini kuwa Yeye ni *Yehova-Yire*, "Bwana akuponyaye"?

163 Sikiliza, rafiki. Mara nyingi sana, huduma yangu huku Marekani haijawa na nguvu sana, kwa sababu inaonekana kana kwamba watu wamechanganyikiwa sa—sana. Mmoja anafundisha jambo moja, na mwingine lingine, badala ya kuketi na kuchukua Biblia na kujisomea mwenyewe, mnaona, na kushawishiwa na Roho Mtakatifu. Sasa, angalieni. Hamhitaji . . .

164 Mmefundishwa, "Watu wanakuwekea mikono." Hiyo ni sawa.

165 Huduma yangu ni kushuhudia ushahidi wa Yesu Kristo aliyefufuka katika wafu.

166 Sasa, baadhi yenu mlifikiri ilikuwa ni telepathia ya kiakili. Mliandika barua zenu leo hii na kusema hivyo. Jana usiku, niliwachukua watu waliokuwa na kadi za maombi, na kuwakatalia, ndipo nikawachukua tu wale wasio na kadi za maombi.

167 Rafiki, hebu nikwambie, kama mtumishi wa Kristo. Hawa hapa Gene na Leo wameketi, rafiki msiri wangu. Huyu hapa Dk. Vayle. Mwanangu, Billy. Kuna Ndugu Sothmann, meneja wa Canada. Ndugu, Ndugu Norman, yule ambaye ameandaa mkutano huu. Wanaume wengi. Pigia mji wangu simu. Mpigie simu meya wa mji, Bw. Hodenpehl. Mpigie simu hakimu. Kipigie simu kikosi cha polisi. Mpigie Dk. Sam Adair, daktari mashuhuri kuliko wote Kusini, kliniki kubwa. Waulize ni maono ya aina gani yanayotokea. Waulize kama ni kweli.

168 Mpigie simu Dk. Sam Adair, usiku wa leo, mwulize yeye hufanya nini anapofika mahali pagumu. Huja nyumbani kwangu, anapiga magoti, na hapo anakaa mbele za Mungu, mimi na yeye, mpaka Mungu atakapoonyesha ono. Mwulize

kama liliwahi kushindwa hata wakati mmoja. Mpigie simu, kwa gharama yangu.

169 Dk. Sam Adair anaendesha kliniki kubwa huko. Mwulize jinsi alivyowahi kupata hiyo kliniki huko. Wakati alipokuwa huko nyumbani kwangu, akilia, na kusema, "Mji huu unahitaji kliniki." Nami nikamwambia mahali ingejengwa hasa, naye angeijenga. Kasema, "Hu—huwezi kupanunua mahali hapo," kasema, "miaka ishirini na mitano kutoka sasa. Iko mahakamani huko Boston."

170 Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI. Itakuwa yako kabla ya saa ishirini na nne." Nikasema, "Utakuwa na kliniki huko, itajengwa kwa matofali mekundu. Utakuwa na ishara mlangoni, na kadhalika, na namna hiyo."

Akasema, "Billy, nisingekutilia shaka bure, mwanangu."

Nikasema, "Bwana amekupa wewe, daktari."

171 Mpigie simu, usiku wa leo, na umwulize kilichotukia. Kesho yake asubuhi akanipigia simu, akasema, "Ninaganda nusura kufa. Ndio kwanza wanipigie simu. Na jambo fulani lilitukia jana usiku, na tayari tumepanunua mahali hapo."

172 Uliza kuhusu wagonjwa anaowatuma kule wakiwa na kansa, wameliwa, hakuna matumaini hata kidogo. Tutamwombea. Wananifukuza hospitalini. Tutaingia chumbani na kufunga mlango. Bwana ataonyesha ono, ama kusema wakati watakapoondoka au kitakachotukia hasa. Mwulizeni kama iliwahi kushindwa.

173 Hili ni dogo tu hapa. Hili ni. . .Hili ndilo dogo zaidi nililowahi kuona likifanyika katika wowote wa mikutano yangu. Hiyo ni kweli. Nimejaribu kila kitu kuvunjilia mbali kitu hicho. Nilikuja, nanyi mkawazia, "kadi za maombi." Nikazigeuza hizo kadi za maombi. Ninajaribu kila kitu. Niko hapa kama mtumishi wenu na ndugu yenu, mambo haya hapa.

174 Huyu hapa Banks Wood ameketi hapa mahali fulani, muuzaji wangu wa vitabu.

175 Leo, Gene, hawa hapa wavulana wawili, mmoja Mkatoliki, na huyo mwingine sidhani alikuwa mfuasi wa lolote. Walipokuja huko Hammond, Indiana, na kumwona Roho Mtakatifu, ndani ya hao maelfu ya watu, wakiita, miaka michache iliyopita. Mmoja wao alifuga ndevu ndefu mno. Walijifanya makachero wa F.B.I. wao wenyewe, washuke waje waone kama mambo hayo yalikuwa ni ya kweli. Wakaja nyumbani kwangu, wakijifanya wainjilisti, na kadhalika. Naye Roho Mtakatifu akashuka moja kwa moja na kuwafichua. Hawa hapa, wameketi hapa sasa. Mnaona?

Kwa nini hamwezi kulistahimili? Kuna nini?

176 Bw. Wood, yuko hapa mahali fulani, alikuwa akiniambia, ameketi papa hapa. Huko chini kabisa Louisiana, nilimwona

akiumia. Nikampigia simu, na kumwambia ajihadhari. Kesho yake, alikikatilia mbali kidole gumba chake. Angaliukatilia mbali mkono wake; Roho Mtakatifu. Siku chache zilizopita usiku, nilipokuwa Chicago, nilimwona katikati ya moshi, na kumwambia awe mwangalifu. Angaliingiwa na sumu ya risasi papo hapo. Na kuingia kwenye lundo hilo la moshi, naye karibu afe papo hapo.

177 Ulizieni jinsi mambo yanavyotabiriwa, majuma baada ya majuma, na miezi baada ya mwezi, kabla hayajatukia.

178 Baadaye, juma hili, nitawaonyesha hii ni nini. Hii ni imani yako mwenyewe; na hiyo ndiyo sababu mambo hayawezi kufanyika. Ni wewe ukivuta kutoka kwa Roho Mtakatifu. Nanii . . . Yesu kamwe hakuona ono kwa ajili ya yule mwanamke. Imani yake ndiyo iliyomgusa. Hiyo ndiyo sababu nguvu zilimtoka. Imani yako ndiyo inayofanya hivyo, si yangu. Wewe ndiwe unayefanya hivyo. Na kama ukiondoa hisia hizo za kimizuka kwako, na kumwamini Mungu kweli, kitu hiki kitatokea kuwa uamsho mmoja mkubwa mno wa haleluya, na vilema, vipofu, viwete, na kila kitu kitatendeka. Lakini mradi mmeketi mkiwa mmejifungia tunduni, Yeye anawezaje kufanya hivyo?

179 Ninaamini katika kuwa mtu wa kutopenda mabadiliko. Lakini, isitoshe, jambo hilo la kutopenda mabadiliko hukupa roho ya ushirikina. Msiniambie. Nimesimama hapa sasa. Ninajua ninachozungumzia. Roho Mtakatifu yuko moja kwa moja humu jengoni sasa hivi, atamponya kila mmoja wenu papo hapo unapoketi, kama mtaamini. Tayari amefanya hivyo. Ni wangapi wanaoamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je, mnaamini hilo? ["Amina."] Vema.

Nitaona jinsi mnavyoamini.

180 Inamisheni vichwa vyenu kwa muda kidogo. Weka mkono wako juu ya mtu aliye karibu nawe. Sasa achana tu na kila ushirikina. Uko chini ya utawala wa Kristo. "Popote walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao."

181 Mnaweza kuniita mnafiki, lakini mtaona baada ya dakika moja. Ninaona watu sasa hivi wakiponywa, hiyo ni kweli, sasa hivi. Huenda usiutambue sasa hivi. Lakini kama wachungaji katika jengo hili hawataona watu wakija kwao baada ya mimi kuondoka, kuwaambia ya kwamba matatizo ya tumbo na mambo kama hayo yaliwaacha, mimi ni shahidi wa uongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ninaliona. Ninalitazama sasa, katika ulimwengu mwingine.

182 Aminini. Aminini. Hakika, kama maskini Mhotentoti asiye na elimu huko Afrika, ambaye hata hajui mkono wake wa kulia au wa kushoto ni upi, anaweza kuukubali, vipi kuhusu wewe unayeweza kusoma Biblia na umefundishwa katika Ukristo?

Kama maskini jamaa huyo hana budi kuamini, kwa kuliangalia mara moja tu, kwa maana sina budi kwenda mahali pengine kesho yake, na maelfu wanainuka kutoka kwenye viti vya magurudumu, na vilema na vipofu, na wewe je?

183 Ee Mungu, jinsi ulivyo na rehema, "Jinsi ulivyo mvumilivu, hupendi mtu yeyote apotee."

184 Sasa keti, umefungiwa ndani pamoja na Mungu. Ungama dhambi yako. Ungama kutokuamini kwako. Mwambie Mungu kwamba unajionea aibu, kwa kutokuamini kwako. Ninakupa changamoto kufanya hivyo, nawe utaona utukufu wa Mungu.

185 Ninajisikia kupakwa mafuta hivi sasa kufanya jambo tofauti na lile nimewahi kufanya. Sijawahi kufanya hivi, maishani mwangu, lakini ninahisi kuongozwa kufanya hivi sasa.

186 Ungama dhambi yako sasa hivi. Unasema, "Vema, mimi ni Mkristo." Ungama kutokuamini kwako. Mwambie Kristo kwamba hutakosa kumwamini tena. Sasa hivi unamkubali. Hivi sasa itaisha. Hutawahi kulilalamikia, tena. Haidhuru linavyoonekana, hisia yake, utaliamini, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Mungu alisema hivyo.

187 Umetoka katika mnara wa Babeli. Umetoka bondeni mahali liliko Yungiyungi la Bondeni. Umefika kwenye mlima, Sayuni, ambapo neema ya Mungu inatiririka bila malipo kutoka kwenye Chemchemi ya Uzima.

188 Ungama makosa yako. Useme, "Mungu . . . " Ikiwa umemfanyia mtu jambo lolote, sema, "Nitarudi na kulisahihisha." Fanya hivyo sasa.

189 Nataka kila mmoja wenu sasa, ninapokariri ombi hili, ninawatakeni mlisali. Litamkeni kwa sauti, pamoja nami. Nitalikariri tu, lakini wewe liombe hilo kutoka moyoni mwako, huku umeinamisha kichwa chako, macho yamefumbwa, kila mtu. Usiinue kichwa chako mpaka nitakaposema hivyo. Ninaangalia tu kuona ninachoweza kuona. Semeni hivi, nyuma yangu:

190 Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa kila zawadi njema, unirehemu, Ee Mungu. Nisamehe kutokuamini kwangu. Ninaiamini Injili. Ninaamini kwamba uko hapa. Ninaamini ya kwamba sasa unatekeleza Neno Lako katika mwili wangu. Fungua mifereji. Ninaondoa kabisa kutokuamini kwangu. Ninampokea Roho Wako. Ninaamini ya kwamba Wewe uko ndani yangu sasa. Ninaamini ugonjwa wangu utatoweka. Mauti na uzima vinawezaje kuwepo katika mwili wangu wakati Wewe uko mle ndani? Nakuamini Wewe. Nami ninakukubali Wewe sasa kama Mponyaji wangu.

Sasa inamisha kichwa chako.

191 Hayo ndiyo maombi yako. Hayo ndiyo maombi yako. Sasa nitakuombea. Endelea kujifungia ndani. Umefungiwa ndani pamoja na Mungu. Usiingize kitu kingine chochote akilini mwako sasa. Yuko pamoja nawe, papo hapo kando yako. Unasema, "Ninataka Roho Mtakatifu, Ndugu Branham." Sawa. Yeye yuko papo hapo kukupa Huyo. Unasema, "Ninataka uponyaji machoni mwangu, Ndugu Branham." Yupo papo hapo kukupa huo. "Nataka mtoto wangu aponywe." Yeye yuko papo hapo kufanya hivyo. "Nataka ndugu yangu, mama yangu." Yeye yuko papo hapo kufanya hivyo, papo hapo. Yehova-yire, Dhabihu iliyotolewa!

192 Sasa nitawaombea. Biblia ilisema, "Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule. Mungu atamwinua." Ikiwa nimepata neema machoni penu, kwa utendaji wa Roho Mtakatifu, nitaomba kwa moyo wangu wote sasa hivi kwamba Roho Mtakatifu akushuhudie kwamba kazi imekamilika.

193 Ee Mungu, Baba yangu, ninakuja katika Jina la Yesu, kuwaombea watu hawa ambao sasa kwa uaminifu na kwa dhati wamekiri makosa yao. Ee Mungu mbarikiwa, huu na uwe usiku ambao hawatausahau kamwe. Jalia Roho Mtakatifu aje katika kila moyo sasa hivi na aondoe tu yote, kila kitu, na magonjwa yote kutoka kwa miili yao.

Sasa namwalika ibilisi kwenye mjadala.

194 Shetani, unajua kwamba umeshindwa. Huna haki za kisheria. Yesu Kristo, Bwana wangu, alikunyang'anya kila mamlaka uliyokuwa nayo, alipokufa pale Kalvari ili kuondoa dhambi na magonjwa. Nawe si kitu ila laghai, na tunakusahi uthibitishe uwezo wako. Unajua kwamba Bwana wetu alipokuja kwenye ule mti, aliulaani huo mti. Kesho yake ulikuwa unanyauka. Ndipo Bwana wetu akawaambia wanafunzi Wake, "Mwaminini Mungu. Kwa maana mkiuambia, mkiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini ulichosema kitatimia, kitakuwa chako."

195 Shetani, unayajua Maandiko juu ya jambo hilo. Na ndiyo kwanza niwafundishe watu hawa, ya kwamba, Mungu yuko ndani yao. Na ikiwa Mungu yuko ndani yao, nao waseme na ugonjwa huo na kusema: "Niondokee," wala wasione shaka moyoni mwao, papo hapo ugonjwa huo hauna budi kuondoka, kwa maana Kristo alisema hivyo. Kwa kuwa, sio wao wanaozungumza. Ni Baba anayekaa ndani yao, ndiye anayezungumza. Ni wahitaji. Kwa hiyo, toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo. Ninasema, kama mtumishi wa Mungu, kwa Ujumbe kutoka kwa Malaika Yule aliyetia mafuta na amewathibitishia watu ya kwamba Yesu yuko hapa na Ujumbe huo ni wa kweli. Kwa hiyo, toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo. Ninakuapisha kumwacha kila mgonjwa na uingie katika giza la nje, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

[Mngurumo wa Upepo Mkali ukienda kasi unapitia jengoni—Mh.]

196 Mliusikia Huo? Nina hakika mliusikia Huo. Ni wangapi waliousikia Mngurumo huo mkuu ukipitia humu jengoni wakati huo? Huyo hapo. Hakika hamtatilia shaka tena. Huyo alikuwa ni Mungu, akijibu. Hivi hamwezi kuona?

197 Inukeni. Je, mnaamini kwamba mmeponywa? Mnaamini kwamba Mungu alijibu maombi? Mwinulieni mikono yenu. Mshukuruni kwa ajili yake. Imekwisha. Umeponywa.

198 Yesu alisema, "Kama *mtauambia*." Ni kitu gani? Unapotoka Babeli, umetoka chini ya kutokuamini. Umetoka chini ya ushirikina. Umetoka chini ya mambo haya yote. Nawe umejazwa na Uzima wa Mungu Mwenyewe. Sauti yako ni Sauti Yake. Ndivyo ulivyo.

199 Nililinena. Chumbani mwangu, muda mfupi uliopita, Mungu aliniambia nifanye hivi. Nalo Hili hapa. Amelithibitisha hivi sasa. Amina. Na Jina la Bwana libarikiwe. Loo, ni wakati wa jinsi gani! Hiyo ni mara ya kwanza kutendeka tangu Afrika Kusini. Mtapapasa-papasa katika kutokuamini hata lini? Mnapata hilo? Upepo ulivuma kwenye jukwaa hili hapa sasa hivi, Roho Mtakatifu alipokuwa akipitia humu, kwa sababu Neno la Mungu lililonenwa ndilo lililofanya hivyo. Amina.

200 Ni wangapi wenu wameponywa? Inueni mikono yenu. Ni wangapi mnajisikia tofauti katika mwili wako? Inua mkono wako. Haya basi. Sasa umeponywa kwa utukufu wa Mungu. Wote wanaojisikia tofauti, ikiwa hukuweza kuusogeza mkono wako, usogeze. Kama ulikuwa huwezi kusikia kutoka kwa sikio lako, weka kidole chako kwenye sikio na usikilize. Unaweza kusikia. Kama hungeweza kutembea, simama kwa miguu yako. Ikiwa wewe ni kipofu, ondoa miwani yako ya jua kutoka kwa macho yako. Unaweza kuona.

201 Roho Mtakatifu alipitia mahali hapa sasa hivi katika thibitisho la Neno. Haleluya! Jina la Bwana libarikiwe. Kitu kama Upepo kilipita juu ya jengo. Ni wangapi wangeweza kuuhisi Huo ulipopitia hapa? Inua mkono wako. Kuwa mwaminifu kwa nafsi yako. Ule Upepo uliopita kwenye hili jengo, huyo ni Roho Mtakatifu. "Liseme, nalo litafanyika." Kama Upepo mkubwa wa upendo ulienda "whiu," moja kwa moja kupitia hapa, nami nikausikia ulipopitia juu ya kusanyiko. Mliusikia na kuuhisi, pia. Ni Uwepo Wake.

202 Wote sasa wanaojisikia tofauti, wote sasa wanaojisikia kuwa mumeponywa, wote sasa wanaohisi kwamba Kristo yu ndani yako!

203 Hiyo ilikuwa ni nini? Kama vile tu Roho Mtakatifu alivyokuja kwenye Siku ya Pentekoste, ameshuka moja kwa moja, Upepo uliovuma hapa. Ni wangapi walio shahidi wa Hilo? Inua mkono wako. Kila mtu, mwaminifu kutoka moyoni mwako.

Huyo hapo. Alipitia humu jengoni kasi papo hapo. Ni Roho Mtakatifu yeye yule. Roho Mtakatifu yeye yule huja kwa Neno lile lile. Jina la Bwana libarikiwe. Amina.

204 Wote wanaoamini kwamba mmeponywa, simameni kwa miguu yenu. Kila mtu anayeamini ya kwamba unajisikia tofauti, naam, kwamba sasa hivi umeponywa, simama kwa miguu yako. Amina. Amina. Ndivyo hivyo. Amina. Wakati wanapongojea, unapoanza kujisikia tofauti! Ikiwa ulikuwa na maumivu ya kichwa, ikiwa yemekwisha, simama. Ikiwa ulikuwa mgonjwa tumboni mwako, simama, ikiwa imekwisha. Simama kama shahidi. Haya basi. Inafanya nini? Roho Mtakatifu ndiye aliyefanya jambo hilo. Amina. Kujazwa na wema Wake! Loo, jamani!

205 "Hii ndiyo hadithi yangu, huu ndio wimbo wangu." Loo, hujisikii vizuri?

> . . . hadithi, huu ndio wimbo wangu,

Kila mtu!

> Kumsifu Mwokozi wangu mchana kutwa:
> Hii ndiyo hadithi yangu, loo, huu ndio wimbo wangu,
> Kumsifu Mwokozi wangu siku nzima.

Hebu tuuimbe tena, kila mtu. Uchukue.

> Hii ndiyo hadithi yangu, loo, huu ndio wimbo wangu,

Kila mtu!

> Kumsifu Mwokozi wangu mchana kutwa:
> Hii ndiyo hadithi yangu, loo, huu ndio wimbo wangu,
> Kumsifu Mwokozi wangu kote . . .

206 Kuponywa kunasikikaje? Mpungieni mikono yenu, jinsi inavyosikika kuponywa. Angalieni tu hapo. Ati mwaniambia ibilisi hajashindwa? Bila shaka, ameshindwa. Amina.

207 Yeye ni wa ajabu. Loo, jamani! Tupe sauti ya, *Wa ajabu, Wa ajabu, Yesu kwangu*. Ni wangapi wanaoujua wimbo huo?

> Wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu
> Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu . . .

Sawa. Unaujua, dada? Sawa.

> Wa ajabu, wa ajabu, Yesu . . .
> Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu Mwenye Nguvu;
> Loo, kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi zote na aibu,
> Wa ajabu, Mkombozi wangu, Jina Lake lisifiwe!

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu kwangu,
Ee, Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni
  Mungu Mwenye Nguvu;
Loo, kwa kuniokoa, kunilinda na dhambi zote
  na aibu,
Mkombozi wangu ni wa ajabu, sifu . . .

208 Kwa faida, kama kunaweza kuwa na mwenye shaka anayesimama karibu, ambaye, ninaihisi moyoni mwangu sasa na dhidi ya Roho yangu. Mtu fulani anafikiri kwamba Mngurumo huo ambao ulipita wakati huo ulisababishwa na ndege au kitu fulani.

209 Mungu, aliye Mwamuzi wangu mkuu, Roho huyo alipitia kwenye jukwaa hili, hata akalipeperusha koti langu ubavuni mwangu, na Akanguruma juu ya hili jengo papo hapo. Nilimhisi, nikamwona, alipotoka. Ni wangapi walio mashahidi sasa? Biblia ilisema, "Kinywa cha mashahidi wawili watatu." Kabisa sio . . . Ni Roho Mtakatifu.

210 Mnakumbuka wakati Yesu alipokuwa akiomba, wakati mmoja, na kukawa na Ngurumo kutoka Mbinguni? Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Ndipo baadhi yao wakasema, loo, jambo fulani, "ngurumo" au kitu kama hicho. Hiyo bado. Roho ya mashaka ingali hai.

211 Lakini, Mungu angali hai, pia. Yuko papa hapa. Upepo ule ule wenye Nguvu Ukienda Kasi ulioshuka kutoka Mbinguni kwenye Siku ya Pentekoste uko papa hapa kushuhudia jambo lile lile tena. Mwenyezi Mungu ndiye Mwamuzi wa mambo yote. Amina.

212 Mnampenda? Bwana asifiwe. Sawa. Kila mtu anyoshe na kupeana mikono wakati tunapoimba tena *Wa Ajabu*. Ninyi Wamethodisti na Wabaptisti mjirekebishe sasa. Vema.

Wa ajabu, wa ajabu . . .

Loo, geuka moja kwa moja, peana mikono na kila mtu aliye karibu.

. . . mimi,
Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
  Mwenye Nguvu;
Loo, kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi
  zote na aibu,
Loo, Mkombozi wangu ni wa ajabu, Jina Lake
  lisifiwe!

213 Bwana asifiwe. Je, mnajisikia vizuri sasa? Kote, mashaka yote yamepita? Mpungieni mikono yenu. "Yote yamepita. Mashaka yote yamekwisha." Loo, jamani! Wa ajabu! Wa ajabu! Vema! "Mashaka yote yamekwisha."

Mungu akubariki, Dk. Vayle.

58-0128 Umoja Wa Muungano
The Hippodrome
Waterloo, Iowa Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org